Taarifa kwa vyombo vya habari
1 Septemba 2015

Wananchi hawana taarifa sahihi kuhusu sekta ya gesi na sera husika
Wengi wanatarajia ajira milioni nne na shilingi milioni 7.5 kwa kila mtu.

1 Septemba 2015, Dar es Salaam: Wananchi wengi hawana taarifa sahihi kuhusu gesi asilia iliyogundulika hivi karibuni nchini Tanzania.

Asilimia 53 wanafikiri kuwa gesi iliyogunduliwa pwani ya Tanzania tayari inavunwa na inazalisha mapato (makadirio yanaonesha kuwa hadi mwaka 2025 ndipo gesi itakapoanza kuvunwa). Pia, wananchi 6 kati ya 10 wanaamini kuwa Serikali na makampuni ya kigeni tayari yameshaanza kuingiza mapato kutokana na gesi hii (kitu hiki kitawezekana pale ambapo gesi itaanza kuvunwa kwa ajili ya matumizi).

Watanzania wanatarajia kwamba kila mwananchi atapata Sh. milioni 7.5 kutokana na gesi katika kipindi cha miaka kumi. Makadirio kaya yanapingana na hali halisi ya mapato ya gesi kwa kila mtu ambayo yanakadiriwa kuwa ni Sh milioni 2.5; hii ni theluthi moja tu ya matarajio ya wananchi. Pia, takriban wananchi 2 kati ya 10 (au 17%) wanafikiri wataajiriwa katika sekta hiyo. Hii ni ishara ya wananchi kuwa na imani kwamba ajira milioni nne zitajitokeza kutoka katika sekta hii ya gesi. Sekta ya gesi nchini Norway hutoa ajira kwa watu 240,000 tu.

Matokeo haya yametolewa na Twaweza katika muhtasari wa utafiti wenye jina la *Matarajio lukuki| Maoni ya wananchi kuhusu sekta ya gesi.* Muhtasari huo unatokana na takwimu kutoka *Sauti za Wananchi*, utafiti wa kwanza barani Afrika wenye uwakilishi wa kitaifa unaofanyika mara kwa mara kupitia simu za mkononi. Matokeo yanatokana na takwimu zilizokusanywa kutoka awamu mbili za kupiga simu. Jumla ya washiriki 1,562 Tanzania Bara (Zanzibar haimo katika matokeo haya) walihojiwa kati ya mwezi Oktoba na Desemba 2013 na, hivi karibuni, washiriki 1,316 walihojiwa kati ya mwezi Aprili na Mei 2015.

Mbali na kupata ajira mpya na fedha nyingi, asilimia 51 wanatarajia gesi asilia italeta umeme wa uhakika (kwa sasa ni wananchi zaidi ya 10% tu waliounganishwa na gridi ya taifa). Asilimia 46 nao wanatarajia gesi ya kupikia itauzwa kwa bei nafuu.

Hata hivyo wananchi wana wasiwasi juu ya mgawanyo wa mapato ya gesi. Wengi wanahofia viongozi wa Serikali (33%) au matajiri (22%) watafaidika zaidi na mapato haya. Mwaka 2013, asilimia 31 ya wananchi walifikiri nchi nzima ingeweza kunufaika kwa usawa, lakini idadi hiyo imeshuka hadi asilimia 22 mwaka 2015.

Serikali ya Tanzania inaandaa sera mbili za kusimamia sekta ya gesi, lakini wananchi 3 kati ya 4 hawafahamu mchakato huu. Asilimia 46 wanataka gesi itumike kuzalisha umeme kwa ajili ya matumizi ya nyumbani, ingawa nusu wengine wametaja suala la kusafirisha gesi kwenda nje.

Wananchi wanadai uwazi na uwajibikaji kwenye maswala ya usimamizi wa rasilimali hii ya gesi asilia. Asilimia 77 ya wananchi wanataka mtu wa kuwapatia taarifa na idadi kubwa zaidi (85%) wanataka taarifa za mikataba kati ya Serikali na makampuni ya gesi ya kigeni yawekwe wazi.

Kuhusu mapato, Watanzania wamegawanyika. Asilimia 55 wangependa serikali ichukue sehemu kubwa ya mapato, wakati asilimia 30 ya wananchi wanataka wawekezaji na Serikali wagawane mapato hayo kwa usawa.

Wananchi watatu kati ya kumi hawajui wamuamini nani kusimamia mapato ya gesi. Wachache (asilima 21) wamelitaja Bunge kama chombo kinachofaa kusimamia mapato ya gesi asilia. Inawezekana Bunge limetajwa kutokana na umaarufu wake wa kuibua kashfa nyingi za rushwa na kusisitiza uwajibikaji wa wahusika hivi karibuni."*Ishara kubwa ya **laana ya rasilimali** hutokea zaidi wakati wananchi hawana taarifa au wana taarifa potofu kuhusu rasilimali hizo. Matarajio yao hayalingani na hali halisi ya sasa au ya baadaye,*" alisema Aidan Eyakuze, Mkurugenzi Mtendaji wa Twaweza. "*Serikali yoyote itakayokuwa madarakani lazima iwe makini kwa kuwapatia wananchi taarifa sahihi, za ukweli, na zenye kuaminika. Wakati wa kushughulikia matarajio ya wananchi ni huu. Katika jambo hili, subira haitavuta heri."*

----Mwisho----

Kwa taarifa zaidi wasiliana na:
Risha Chande
Mshauri Mwanadamizi wa Mawasiliano, Twaweza
e: rchande@twaweza.org | **Simu:** (+255) (0) 656 657 559

Maelezo kwa Wahariri

- Ripoti nzima, pamoja na mifano ya majaribio yaliyotumika vinapatikana www.uwezo.net ww.twaweza.org au www.twaweza.org/uwazi
- Twaweza inafanya kazi kuwezesha watoto kujifunza, wananchi kuwa na utayari wa kuleta mabadiliko na serikali kuwa wazi zaidi na sikivu katika nchi za Tanzania, Kenya na Uganda. Tuna programu, wafanyakazi na ofisi katika nchi zote tatu, na utaratibu unaoheshimika kimataifa wa kujifunza, ufuatiliaji na tathmini. Programu zetu muhimu ni pamoja na *Uwezo*, tathmini kubwa ya kila mwaka ya wananchi barani Afrika inayopima viwango vya watoto vya kujifunza kwenye maelfu ya kaya, na *Sauti za Wananchi*, utafiti wa kwanza Afrika wenye uwakilishi wa kitaifa unaofanyika kwa njia ya simu ya mkononi. Pia tunashiriki kwenye masuala ya umma na sera, kupitia ubia wetu na vyombo vya habari, juhudi za kimataifa zinazoshughulikia masuala ya uongozi kama vile mpango wa Ushirikiano na Serikali wazi (OGP).
- Unaweza kufuatilia kazi za Twaweza kupitia:
  Tovuti: www.twaweza.org **Facebook:** Twaweza Tanzania **Twita:** @Twaweza_NiSisi